


Muhtasari

- Mvua za *Msimu* zimeanza kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka na wakulima wanaendelea kuandaa mashamba na kupanda
- Mvua zinazotarajiwa kwa kipindi cha tarehe 1 -10 Disemba 2018 zitasaidia katika uoteshaji na kukua kwa mazao
- Wakulima wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za siku kumi na kufata ushauri wa maafisa ugani kwa matumizi stahiki ya mvua zinazotarajiwa
- Wafugaji wanashauriwa kutumia vizuri maji pamoja na malisho ya wanyama.

**MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA
KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2018**

Katika kipindi hicho, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilipelekea kusukumwa kwa ukanda wa mvua wa ITCZ hadi kufika katika nchi yetu. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilishamiri katika eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi na hivyo kusababisha migandamizo midogo ya hewa. Eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kulikuwa na joto la bahari la wastani hadi chini ya wastani. Hali hii ilipelekea kuongeza kwa upepo uvumao kutoka magharibi hivyo kuimarisha mifumo ya mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi



Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Novemba 21- 30, 2018

**MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA
NOVEMBA 21-30, 2018**

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita, baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka yaliendelea kupata mvua za msimu wa Vuli, ambazo zilikuwa kidogo na mtawanyiko hafifu. Mvua za kiwango cha kati ya 26 mm - 100mm zilipatikana katika maeneo machache ya kanda ya ziwa Victoria, baadhi ya sehemu za nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja visiwa vya Unguja na Pemba.

Kwa upande wa maeneo yanayopata mvua msimu mmoja kwa mwaka vipindi kadhaa vya mvua viliripotiwa ambapo kiasi cha 26 mm – 100 mm za mvua zilirekodiwa katika maeneo mengi ya magharibi mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi na Kanda ya kusini kama inavyoonekana kwenye kielelezo.

**TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA
KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2018**

Katika kipindi cha dekadhi husika, wakulima katika maeneo mengi nchini waliendelea na uandaaji wa mashamba pamoja na upandaji kutokana na mvua za *Vuli* zinazoendelea na kuanza kwa mvua za *Msimu*. Hata hivyo maeneo machache yanayopata msimu mmoja na yale ya misimu miwili ya mvua hususan maeneo ya Longido, Mtwara na Shinyanga bado wanaandaa mashamba kutokana na kuchelewa kuanza kwa mvua na mtawanyiko hafifu.

Hali ya mazao ya mahindi na maharagwe kwa mkoa wa Kagera, yanaendelea vizuri na katika hatua ya kukomaa na wakulima wanaendela na shughuli za palizi kwa mazao yaliyochelewa kupandwa.

Hali ya upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo yameimarika katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka kutokana na mvua za *Vuli* zinazoendelea.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2018

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kupungua katika maeneo mengi ya nchi kutokana na mtawanyiko hafifu wa mvua..

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2018

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii inatarajiwa kupelekea kusukumwa kwa ukanda wa mvua wa ITCZ na kuwepo katika nchi yetu. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi na hivyo kusababisha matukio ya vimbunga hasa katika kipindi cha siku tano za mwisho. Eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la chini ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuongezeka kwa upepo uvumao kutoka magharibi hivyo kuimarisha mifumo ya mvua katika eneo la magharibi mwa nchi

HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2018

Katika kipindi cha siku kumi zijazo kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) na nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) yanatarajiwa kuwa na mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) na pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) inatarajiwa kuwa na mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo hasa siku tano za mwisho.

Kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) na magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) inatarajiwa kuwa na mvua zinazoambatana na ngurumo hasa katika baadhi ya maeneo.

MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10,2018

Mvuua zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja na miwili ya mvua zinatarajiwa kuongeza unyevunyevu kwenye udongo kwa uoteshaji wa mbegu na ukuaji wa mazao. Wakulima wanashauriwa kuendelea kufatilia taarifa za siku kumi na kufata ushauri wa maafisa ugani kwa matumizi stahiki ya mvua zinazotarajiwa. Hata hivyo wakulima wa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka wanashauriwa kuzitumia mvua za *Msimu* zinazotarajiwa kupanda mazao pale kutakapokuwa na unyevunyevu wa kutosha kwenye udongo. Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuzingatia ushauri wa maafisa ugani katika maeneo yao.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2018.

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa vya wastani katika sehemu nyingi nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji kwa uangalifu kwa matumizi endelevu ya rasilimali hii.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania